

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE



OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR
(ADMINISTRATION & FINANCE)

P.O. BOX 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA

TELEPHONE: +255 023 2640006-9, Direct +255 023 2640023,

FAX: +255 023 2640016. TELEGRAMS: UNIAGRIC - TELEX: 55308

E-mail: dvcadminfin@suanet.ac.tz

Kumb. Na. SUA/ADM/K.1/6 VOL. II

Tarehe: 20/04/2018

Wanachama wote wa Mfuko wa Afya wa
Jumuiya ya SUA (SCHF)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
MOROGORO

YAH: UHAKIKI WA WANACHAMA WA SUACHF NA UTENGENEZAJI WA VITAMBULISHO VIPYA

Kichwa cha habari hapo juu kinahusika.

Mtakumbuka kwamba Mwongozo wa Mfuko wa Afya wa SUA ulipitiwa upya ili kukidhi matakwa ya kisheria na maelekezo ya SSRA. Mwongozo huo uliidhinishwa na mkutano maalum wa wanachama wa Mfuko uliofanyika tarehe 24 Aprili, 2017 na Baraza la Chuo katika mkutano wake wa 147 uliofanyika tarehe 29 Juni, 2017; na baadaye kuwasilishwa "SSRA".

Imethibitika kwamba vitambulisho vingi vya wanufaika wa SCHF vimekwisha muda wake; aidha kuna baadhi ya wafanyakazi walikwishapoteza sifa za uanachama kwa sababu mbalimbali lakini bado wanamiliki kadi za vitambulisho na kuendelea kutumia huduma za Mfuko kinyume cha taratibu.

Kamati ya Kusimamia Mfuko katika mkutano wake wa 46 uliofanyika tarehe 16 Machi, 2018 pamoja na mambo mengine uliamua kuwa lifanyike zoezi la uhakiki wa wanachama kwa kujaza fomu upya za usajili, kwa mujibu wa Mwongozo mpya kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- i) **Wanufaika**
 - Mwanachama mchangiaji
 - Mume/Mke, na watoto/wategemezi wanaotambulika kisheria wasiozidi wanne
- ii) **Mahitaji**

Picha za wahusika na Hati ya Mshahara ya hivi karibuni kwa minajiri ya uhakiki
- iii) Zoezi la ujazaji fomu litaanza tarehe 10 Mei, 2018 na kukamilika tarehe 31 Julai, 2018.
- iv) Fomu za usajili zitapatikana kwenye tovuti na kwenye Ofisi ya Vitambulisho
- v) Kuanzia tarehe 1 Agosti, 2018 vitambulisho vya zamani havitatumika.

Nawatakia utekelezaji mwema,


Prof. Yonika M. Ngaga

**NAIBU MAKAMU WA MKUU WA CHUO
(UTAWALA NA FEDHA)**

Nakala: Makamu wa Mkuu wa Chuo
" Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Taaluma) } ndani ya jalada
" Mbao za matangazo
" Kwenye mtandao